KISWAHILI GREDI YA SABA

KUSIKILIZA NA KUJIBU

Vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza mazungumzo

- Kusikiliza kwa makini
- Kumtazama mzungumzaji
- Kutikisa kichwa
- Kutumia vihisishi
- Kuepuka vizuizi vya mawasiliano

Vipengele vya kuzingatia katika kujibu mazungumzo

- Kutumia lugha ya adabu
- Kutomkata mzungumzaji anapozungumza
- Ubadilishanaji zamu ufaao
- Kujibu kwa kujikita katika kiini Cha swali

MSAMIATI WA UFAHAMU

Eleza maana ya maneno yafuatayo

Kujinadhifisha- Ina maana sawa na kujing'arisha _ Hali ya kujisafisha uwe msafi

Taharuki – kuwa na hamu ya kutaka kujua kitu kitakachotokea baadaye

Kitana- kifaa Cha kuchana nywele

Wakanawa- ni kuosha mikono kwa kutumia maji

Kudadisiwa- peleleza jambo kwa kuulizauliza maswali

Eleza maana ya vifungu vifuatavyo

Msafiri ni aliye bandarini- Ina maana mambo kuwa tayari kwa jambo Fulani

Siku njema huonekana asubuhi – Ina maana kuwa kufanikiwa kwa jambo Fulani huonekana mwanzoni.

Mguu niponye- kukimbia mbio sana ili kujinusuru

Kuwa na moyo wa simba- ni kuwa jasiri

Kuangua kucha- ni kukata kucha-

VIAKIFISHI